# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA

**09 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 09 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**262 MHESHIMIWA ATUPELE FREDY MWAKIBETE (BUSOKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya Mpata, Isange na Ntaba - Busokelo.

**263 MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza kuwawezesha Maafisa Ugani kwa kuwapa mafuta ili waweze kutembelea Wakulima.

**264 MHESHIMIWA DKT. ANGELINA SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Shule za Msingi ambazo hazina uzio maeneo ya Mijini.

**265 MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Barabara za Mitaani zinafanyiwa ukarabati na maboresho ili kuepusha usumbufu wakati wa mvua.

## WIZARA YA KILIMO:

### 266 MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji Bonde la Rukwa wenye thamani ya Shilingi Bilioni 21 utakamilika.

### 267 MHESHIMIWA SALIM MUSSA OMAR (GANDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, upi mpango wa Serikali kuifanya NFRA kujitegemea ili kuepuka uhaba wa chakula pindi nchi tegemezi zinapokumbwa na majanga.

## WIZARA YA UJENZI:

### 268 MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mkiu - Liganga - Madaba utaanza kwa kiwango cha lami kwani uwekezaji wa Liganga upo mbioni kuanza.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**269 MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini mpango wa Ujenzi wa Chuo cha Utalii katika Mji wa Njombe utaanza.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**270 MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga Kiwanda cha Chai cha Kilolo.

**271 MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka unakamilika.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**272 MHESHIMIWA ABDI HIJA MKASHA (MICHEWENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha Kituo cha TEHAMA kilichopo Wilaya ya Micheweni.

**WIZARA YA MAJI:**

**273 MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini usambazaji wa maji ya Ziwa Victoria katika Kata za Mondo, Busangwa, Sekebugolo na Mwasubi - Kishapu utakamilika.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** — **BARAKA I. LEONARD**
**09 MEI, 2025** — **KATIBU WA BUNGE**